

## Maswali na Majibu

1. Peana mifano 2 iliyofanya ndugu zake Yusufu wawe na wivu.  
*Yakobo alimpa koti lililokuwa la kawaida. Aliota kwamba watamwinamia.*
2. Ndugu zake walimfanyia mambo gani 2 ya kikatili?  
*Walimtupa kwa shimo. Walimuuzua kama mtumwa.*
3. Nani alinunua Yusufu kule Misri? Mbona alimtupa Yusufu gerezani?  
*Potifa aliyekuwa nahodha wa jeshi la Misri. Mke wake alidanganya eti Yusufu alitaka kufanya ngono naye.*
4. Mnyweshaji aliota eti nini alipokuwa gerezani? Hiyo ndoto ilimaanisha nini?  
*Alimimina vifurushi 3 vya mizabibu kwa kikombe na akampa Farao. Baada ya siku 3 ataachiliwa na awe mnyweshaji wa Farao tena.*
5. Mwokaji aliota nini? Ndoto yake ilimaanisha nini?  
*Ndege walikula mikate kutoka kwa vikapu 3 kutoka kwa kichwa chake. Baada ya siku 3 atakufa.*
6. Farao aliota eti nini? Hizo ndoto zilimaanisha nini?  
*Ng'ombe 7 wembaba walikula ng'ombe 7 wanono. Masuke 7 ya nafaka nyembaba ilikula masuke 7 nono. Miaka 7 ya mavuno mazuri na miaka 7 ya njaa.*
7. Yusufu alifanya nini kwa miaka 7 ya mavuno mazuri. *Aliweka chakula kingi.*
8. Ndugu zake Yusufu walitimiza ndoto zake namna gani walipokuja Misri?  
*Walimwinamia.*
9. Yakobo na familia yake walienda kuishi wapi wakati wote wa njaa?  
*Gosheni kwa nchi ya Misri.*
10. Mbona haya mambo yote yalitendeka kwa Yusufu?  
*Ili aponyeshe familia yake kwa kuwapa chakula wakati wa njaa.*

## Mistari ya kukariri

Mwanzo 50:20 Warumi 8:28 Waebrania 11:22

## Mazungumzo

Eleza vile Mungu alitumiza mambo hayo yote mabaya kwa Yusufu ili aokoe watu wake wateule – Familia ya Yakobo.

## Kuandika

Andika juu ya ndoto moja kutoka kwa hii hadithi na ueleze vile ilikuja ikawa ya kweli

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM



## Somo la 11 Yusufu anaokoa familia yake

**SOMA Mwanzo 37:2 – 28; 41:28 – 40; 45:25 – 28; 50:22**

### SOMO

Yakobo na familia yake waliishi kwa nchi ya Kanaani (iliyoitwa Israeli baadaye). Hii ni nchi yenye Mungu aliahidi Ibrahimu, Isaka na Yakobo na familia yao milele. Yakobo alikuwa na wana 12 lakini alimpenda Yusu zaidi ya wana wengine. Yakobo alipea Yusufu koti lililokuwa la kipekee kuonyesha kwamba alikuwa amempenda zaidi. Hii ilifanya ndugu zake kuwa na wivu.

Yusufu alikuwa na ndoto mbili. Ndoto ya kwanza ilikuwa juu ya miganda (vifurushi) vya ngano. Ndoto ya pili ilikuwa juu ya jua, mwezi na nyota. Ndoto zote mbili zilikuwa na maana moja. Ndoto zote zilikuwa na maana kwamba wakati ujao ndugu zake 11 watamwiinamia. Yusufu alipowambia juu ya hizo ndoto, ndugu zake walikuwa na wivu zaidi.

Yakobo alituma wana wake wakubwa 10 huko Shekemu kuchunga kondoo. Baadaye Yakobo alituma Yusufu kuwajulia ndugu zake hali. Wale ndugu zake walipomwona Yusufu anakuja, waliamua kumuua. Lakini mmoja wao aliyeitwa Reubeni alisema, "Tusimue Yusufu. Tumtupe ndani ya shimo." Kwa hivyo walimtupa ndani ya shimo. Reubeni alikuwa na mpango wa kumwoko Yusufu baadaye, lakini kwanza alienda kuangalia kondoo.

Muda wenye Reubeni hakukuwepo, wafanyi biashara walifika. Ndugu wenye walikuweco walimuuzua Yusufu kwa wale wafanyi biashara kwa vipande 20 vya fedha. Wale ndugu walichukuwa lile koti nzuri la Yusufu na kumwagia mwagia damu. Walienda na kumwambia baba yao kwamba Yusufu aliuawa na wanyama wakali. Yakobo alihuzunika na kuwa mwenye fedheha.



Nyumba ya tajiri huko Misri

Yusufu alipelekwa Misri na kuuzwa kwa mtu aliyeitwa Potifa. Potifa alikuwa nahodha wa jeshi la Misri. Baada ya muda mfupi, Potifa aliona Yusufu ni mzuri na mwaminifu na akamweka kuwa msimamizi kwa nyumba yake.

Yusufu alikuwa na sura nzuri na mke wa Potifa alimshawishi wawe wapenzi na walale naye. Yusufu alikataa na hiyo ilimkasirisha mke wa Potifa. Akamwambia Potifa, “Yusufu alinilazimisha nilale na yeye.” Potifa alikasirika na kutupa Yusufu gerezani.

Kwa muda mfupi, mkubwa wa gereza aliona kwamba Yusufu alikuwa kijana mzuri tena mwaminifu na akamweka kuwa msimamizi wa wafungwa wenzake. Farao alikuwa amewaweka watumizi wake wawili ndani ya gereza: mnyweshaji (aliyekuwa wakushugulika divai) na mwokaji.

Usiku moja mnyweshaji na mwokaji walikuwa na ndoto. Waliota kwamba walikuwa wanafanyia Farao kazi tena. Walifadhaika sana na hizo ndoto zao kwa hivyo wakauliza Yusufu maana ya hizo ndoto.

Mnyweshaji aliota kwamba kulikuwa na vifurushi vitatu vya mizabibu. Aliziokota na kukamlika ndani ya kikombe cha Farao na akampa Farao. Yusufu alimtafsiria kwamba baada ya siku tatu ataachiliwa kutoka gerezani na atarudi kumfanyia Farao kazi tena. Mnyweshaji aliahadi kwamba ataambia Farao juu ya Yusufu.

Mwokaji aliota kwamba alikuwa amebeba vikapu vitatu vya mikate kichwani akipeleka kwa Farao. Ndege walikuja na wakala hizo mikate. Yusufu alimwambia mwokaji kwamba baada ya siku tatu, atanyongwa. Atakufa na ndege watamkula.

Baada ya siku tatu mwokaji alinyongwa. Mnyweshaji alienda kufanyia Farao kazi tena lakini alisahau kumwambia Farao juu ya Yusufu. Ilikuwa jaribio kubwa sana kwa Yusufu. Mungu alikuwa amemsahau?

Baada ya miaka miwili, Farao aliota ndoto mbili na akafadhaika na maana ya hizo ndoto. Mnyweshaji alikumbuka na akamwambia juu ya Yusufu. Alisema kwamba Yusufu anajua maana ya ndoto. Yusufu alitolewa kwa gereza na kupelekwa kwa Farao. Yusufu aliwambia kwamba Mungu huwa anamwambia maana ya ndoto.

Farao alikuwa ameota kwamba ng’ombe wembamba saba walikula ng’ombe wanono saba. Tena akaota kwamba masuke saba membamba yalikula masuke saba manono. Yusufu alimwambia kwamba hizo ndoto zilikuwa na maana moja. Kutakuwa na miaka saba ya mavuno mazuri. Baadaye kutakuwa na miaka saba ya njaa.

Yusufu aliambia Farao kuchagua mtu wa hekima atakayeweka chakula kingi wakati wa mavuno mazuri ili kuwe na chakula cha kutosha kwa hizo miaka za njaa. Farao aliamua kupea Yusufu hiyo kazi. Yusufu alifanywa kuwa mtawala wa Misri. Mungu aliwezesha kuwa na miaka saba ya mavuno mazuri tena miaka saba ya njaa. Njaa ilikuwa kubwa lakini Misri ilikuwa na chakula cha kutosha kwa maghala yenye Yusufu aliweka. Yusufu aliuzia Wamisri na hata wageni waliokuja kununua chakula kutoka kwa hizo maghala.

Njaa ilikuwa nyingi kwa nchi ya Kanaani yenye Yakobo aliishi pamoja na familia yake. Yakobo alituma ndugu zake Yusufu kule Misri ili wanunue chakula. Lakini hakukubali Benyamini aende kwa sababu alikuwa ndiye alikuwa mdogo kwa wana wake.

Ndugu wa Yusufu walipowasili, walipelekwa kwa Yusufu. Hawakumtambua Yusufu kwa vile alikuwa mtawala na mavazi ya Misri. Walimwinamia. Hii ilitimiza ndoto yenye Yusufu aliota juu ya miganda ya ngano na jua, mwezi na nyota. Yusufu aliwajaribu ndugu zake ili aone kama wangali wakatili tena waovu. Aliwambia, “Nyinyi ni wapelelezi.” Aliwaweka gerezani kwa siku tatu. Halafu akawaita tena na kuwauzia ngano. Lakini alimwacha Simon gerezani. Aliwambia lazima wakirudi kuja kununua chakula Misri, waje na ndugu wao mdogo Benyamini.

Baada ya muda chakula kiliisha. Yakobo hakutaka Benyamini aende Misri lakini wanawe walimshawishi na akakubali wakaenda. Walipofika Misri, Yusufu aliwajaribu tena na kuwatisha kwamba atamtupa Benyamini gerezani. Lakini Yuda alijitolea kwenda gerezani badala ya Benyamini ili Yakobo asikasirike sana. Yusufu alipoona kwamba ndugu zake wamebadilika na ni wazuri, alijitambua, “Mimi ni ndugu yenu, Yusufu.” Ndugu zake walisikitika sana kwa ukatili waliomfanyia Yusufu.

Yusufu aliwapea ndugu zake chakula na wakasafiri kurudi nyumbani. Walimwambia Yakobo kwamba walikuwa wamempata Yusufu. Halafu walienda wote Misri ili wawe karibu na Yusufu akiwapa chakula cha kutosha. Farao aliwapea sehemu ya kuishi kule Misri. Hiyo sehemu iliitwa Gosheni.

Yusufu alikuwa na shida nyingi sana katika maisha yake: aliuzwa kama mtumwa, aliwekwa gerezani, mnyweshaji alimsahau. Lakini Yusufu hakusahau kwamba Mungu alikuwa naye. Yusufu aliendelea kuwapa familia yake na watu wengine chakula kwa hizo miaka saba za njaa. Yusufu aliamini kwamba hayo yote yalitendeka ili aokoe familia yake.



Mungu aliahidi kwamba wazao wa Yakobo (taifa la Israeli), siku moja watarudi Kanaani. Yusufu aliamini Mungu. Yusufu aliambia wana wake, “Mkirudi Kanaani, nataka muende na mifupa yangu mkanizike kule.” Hiyo ni imani kweli kwa ahadi za Mungu.